# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA TISA

**23 SEPTEMBA, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 23 SEPTEMBA, 2022

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**134. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Wastaafu ambao Waajiri wao walikuwa hawatoi michango katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii watalipwa haki zao.

**135. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Waajiri ambao wanasuasua katika kuwaajiri Watu wenye Ulemavu wenye sifa stahiki.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**136. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubebea Wagonjwa katika Kituo cha Afya Gidas.

**137. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka CCTV Kamera na *alarm system* katika masoko, shule na sehemu za wazi zenye mikusanyiko.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**138. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni kwanini Serikali isiteue Majaji wa muda mfupi *(Acting Judges)* ili kusikiliza kesi za mauaji zinazochukua muda mrefu.

**139. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupitia upya Mfumo wa Haki Jinai ili kupunguza idadi kubwa ya Mahabusu Magerezani.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**140. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhusu mpango wa kukuza uchumi wa bluu kwa kuzingatia mazao yatokanayo na Bahari.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**141. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itarudisha huduma ya treni Manyoni – Singida.

**142. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (UKONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Pugu – Kifuru hadi Mbezi Mwisho kwa kiwango cha lami.

## WIZARA YA KILIMO:

**143. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usajili wa Wakulima wa mazao ya kimkakati ikiwemo Pamba, Korosho, Kahawa, Chai na Michikichi.

**144. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Wilayani Muleba.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**145. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni Vivutio gani vya Utalii vimetambuliwa Wilayani Ukerewe na hatua zipi zimechukuliwa kuendeleza na kuvitangaza.

**146. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha Hifadhi ya Kitulo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**147. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Wananchi wa Kata ya Makurunge watapatiwa eneo la Makazi la Razaba baada ya maeneo yao kuchukuliwa.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**148. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Minara ya Mawasiliano itajengwa katika kata za Endanywish, Endagulda Gidurgadaw, Yaeda Ampa, Hayeda na Endanilay.

**149. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga Minara ya Mawasiliano katika Kata za Ikoma, Roche, Gobire na Bukura.

**WIZARA YA NISHATI:**

**150. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la umeme la Mto Lumakalya Wilayani Makete.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**151. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha uwekezaji wa miradi 294 yenye thamani ya Dola Bilioni 8.04 inatekelezwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**152. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuvuna maji katika Mji wa Itigi.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**153. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni kwa nini kesi 1,097 za kodi zenye thamani ya shilingi Trilioni 360 na Dola za Marekani milioni 181.4 hazijaamuliwa hadi sasa

## III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022];*

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022;

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022; na

Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022.

**IV. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

**V. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**

**VI. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**23 SEPTEMBA, 2022** | **KATIBU WA BUNGE**